

MRADI WA TASAF MKOMBOZI KWA KAYA MASKINI

Mratibu wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini(TASAF III) wilayani Kilosa Bw. Dedan Maube ametoa wito kwa jamii na hasa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini watambue kuwa msingi/Roho ya mafanikio ya mpango huo ni utimizaji wa masharti ya Elimu na Afya.

Dedan amesema hayo hivi karibuni kwa wanakamati wa mpango huo toka katika vijiji mbalimbali wilayani Kilosa na kusisitiza kuwa walengwa wanapaswa kuhakikisha watoto wanahudhuria masomo kwa zaidi ya asilimia 80 katika kipindi cha miezi miwili. Hivyo amewataka wanakamati hao kuwakumbusha walengwa kuhakikisha watoto wanaotakiwa kuhudhuria kliniki wanahudhuria mara mbili katika kipindi husika.

Akifafanua zaidi amesema ruzuku ya Elimu inatolewa kwa wanafunzi wanaosoma shule ya msingi kuanzia elimu ya awali hadi darasa la saba kwa kila kaya yenyewe watoto zaidi ya wanne kila mtoto hupata shilingi 2000, shule ya msingi watoto zaidi ya wanne kila mtoto ni shilingi 2000, wakati elimu ya sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne watoto zaidi ya watatu kila mtoto shilingi 4000/ na wanaosoma kidato cha tano hadi cha sita wasiozidi wawili ni shilingi 6000 kwa mtoto mmoja.

Sambamba na hayo Maube amesema kuwa dhumuni la ruzuku hiyo ni kuwawezesha watoto hao kupata huduma za Afya, na kumudu gharama za shule ikiwa ni pamoja na kulipia michango midogo midogo.

Kwa niaba ya walengwa wenzao wa mradi huo kwa nyakati tofauti Bi Coleta Katomondo wa Ruaha na Bw. Paulo Ilehao wa kijiji cha Kiduhi wilayani hapa wamesema mradi huo kwao ni mkombozi kwani pesa hizo zimewasaidia sana na kuwawezesha kununua vyakula,kulima mashamba, kufungua miradi mbalimbali midogomidogo,kununua mahitaji ya shule kwa watoto wao kama vile sare za shule na kadhalika lakini pia umewawezesha kununua mabati kwa ajili ya ujenzi, hivyo wanaushukuru uongozi wa Wilaya kwa kuwatazama kwa jicho la karibu na wanaomba wilaya isiwachoke kuwasaidia kujikwamuia katika umaskini.